# Bado

**Harmonize**

Aaaah
Kutwa kidomo wazi, nikifuta na machozi
Huku namuomba Mola unitoke moyoni
Ila ndo siwezi, nakesha ka mlinzi
Maana hata nkilala unaniijia ndotoni
Lato, asante kwa kuniumiza
Nimejifunza mengi, mwanzo sikuyajua
Katu, naapa kutolipiza
Ila mwambie mapenzi abaki kuyasikia, eeeh eeeh
Nakumbuka maneno yako
Hutonikimbia, utabaki namiii
Tena ukala na viapo, Taurat, Bibilia
Leo sikuoni

Ila mwenzako bado
(Bado bado, bado bado)
Mwambie bado
(Bado bado, sijapona)
Ila mwenzako bado
(Bado bado, bado bado)
Mmh bado
(Bado bado, sijapona)
Misijapona roho

Mmhh mmh
Aa-ah Mola nishike mkono Baba Muumba
Haya ninayoyaona, simanzi
Ah, yaani bora jicho mchanga ningefumba
Huenda ningeshapona, maradhi
Oh maumivu yangu, hayawezi kupona kwa vidonge
Sababu panaponichoma, nikipapasa sipaoni
Kweli peke yangu, umeniacha na unyonge
Kabisa wakanipokonya tonge langu mdomoni

Onana, nakumbuka maneno yako
Hutonikimbia, utabaki namiii
Oh, mi ndo mwili, mi roho yako
Yaani umetimia, mbona sikuoni
Ila mwenzako mimi

(Bado bado) Mmh Mmh (bado bado)
Mwambie bado
(Bado bado, sijapona)
Ila mwenzako bado
(Bado bado, bado bado)
Mmh bado
(Bado bado, sijapona)

Ah Aah Ile roho yangu mama
(Ibebe)
Inandondoka
(Ibebe)
Iokote mama
Ibebe, Chaukucha nsije zima
Ooh roho yangu
(Ibebe)
Inandondoka

(Ibebe)
Njoo unishike mama ooh
(Ibebe, Chaukucha nsije zima)
Ah aah, ai wewe
(Ibebe)
Watanizika mama
(Ibebe)
Mwenzio taabani
(Ibebe, Chaukucha nsije zima)

Mmh
Masikini pendo langu
(Ibebe)
Linandondoka
(Ibebe)
Niokote mama
(Ibebe, Chaukucha nsije zima)

Ibebe, ibebe
Ibebe, Chaukucha nsije zima
Ibebe, ibebe
Ibebe, Chaukucha nsije zima


Sponzor: www.srovnavac.cz - vyberte si pojištění online!